# Jarida la UQAB

Toleo 45 - Safar 1442 H / Oktoba 2020 M

## MABADILIKO NA USHINDI WA KWELI UPO KATIKA KUJIFUNGA NA ULINGANIZI WA KHILAFAH SIO MAKUNDI YA HUSTLER NA DYNASTY







# TOLEO

**Leo hii Imarat na Bahrain wanatia saini ya Mkataba kati yao na Utawala wa Kiyahudi, Uhaini Mkuu kwa Palestina Eneo la Safari ya Mtume (saw) ya Isra na Miiraj… Hata Bila ya Kumhofu Allah wala Mtume Wake wala Waumini!**

Imeripoti France24 jana 14/9/2020M kua (Mashariki ya kati, Jumanne itaingia kwenye mkondo mpya, ambapo utawala wa Bahrain na Milki za Imarati zitatia saini mkataba wa makubaliano na Israel huko Washington…. na yatarajiwa kusimamiwa na Rais wa Amerika Donald Trump, katika sherehe itakayofanyika White House juu ya saini hiyo… na wajumbe wawili wa Kiarabu, wataongoza mawaziri wa mambo ya nje wa nchi mbili za Kikhaliji…) yaani, ni kwamba Imarati na Bahrain leo Jumanne huko katika mji Mkuu mweusi Washington watatia saini makubaliano ya khiyana kuu kwa mahali ilipokua Israa ya Mtume (saw) na Miiraj yake, pasi na kumuogopa Allah, Mtume wake na wala Waumini! Nao kwa kufanya hivyo, watakua wamefuata mwenendo wa mfano wao kabla yao: serikali ya Misri katika mkataba wa Camp David, PLO huko Oslo na serikali ya Jordan katika Waadi Araba!

Hakika watawala katika miji ya Waislamu, kabla ya mikataba hii na baada yake walikua wakiamiliana na serikali ya Kiyahudi. Lakini wakifanya hivyo nyuma ya pazia, huku wakichunga japo kidogo haya, bali uoga. Na ilipoondoka hicho kizibo, imekua sasa kutangaza wazi hayo makubaliano ni jambo la kifahari kwao. Wanatangaza wazi hili bila ya kuhisi unyonge au hata



angalau aibu kidogo au haya! Na unyonge huu hakuna budi utawafika tu! Wakubali hilo au wakatae, huo ndio mwisho wa mhalifu yeyote katika haki ya Dini yake au Ummah wake.

سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ

"Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya" [Al-An'am: 124].

Kwa hakika ni moja kati ya makubwa, kutokea hili linalotokea! Ambapo mapatano yanaendelea kwa kasi hii, huku Ummah na majeshi yake wakiangalia na kusikia, bila ya majeshi ya Waislamu kutikisika na kuwapindulia dunia juu yao na kuwaondoa! Kisha na wale ambao bado hawajatia saini mikataba ya wazi hawana tofauti yoyote na waliotia saini. Kwani Oman hukaribisha na kukaribishwa na utawala wa Kiyahudi. Nayo Qatar ndio wa kati (aso na mapendeleo) kati ya Mayahudi na Ghaza! Na utawala wa Saudi katika miji ya Hijaaz, nao anga zake zi wazi kwa ndege za utawala bandia na uliokalia kimabavu Al-Qudsi tukufu ya Waislamu! Kisha nao watawala wa Uturuki, bado unautambua utawala wa Kiyahudi uliokalia kimabavu Falastin! Ama kiukweli ni moja ya makubwa kutokea hili linalotokea, kana kwamba ni jambo la kawaida kati ya ndugu wa tumbo moja! Na kana kwamba sio zaidi ya tofauti ndogo tu ya kimtazamo kuhusu mipaka!

**Enyi Waislamu:** Hakika ardhi barikiwa ya Palestina, ardhi iliyokua mafikio ya safari ya Israa na Miiraj, imo ndani ya nyoyo za Waislamu. Hata kama wameonjwa kwa watawala Ruwaibidhwa (wenye akili ndogo) wanaowatii makafiri wakoloni, zaidi ya kumtii Mola wa viumbe! Hakika Palestina na Qudsi yake ni Palestina ya Waislamu wala Palestina sio ya hao watawala wasaliti, wala Qudsi si yao! Na kusawazisha mahusiano kati yao na serikali ya Kiyahudi iliyoinyakua Palestina kimabavu, wote watahitimishwa na udhalili na aibu mpaka siku yao walioahidiwa. Kwani hakika, Palestina itarudi kwa wenyewe baada ya kupigana na Mayahudi wanyakuzi wa ardhi iliobarikiwa, katika siku ambayo itakayoshuhudiwa, itakayofunikwa na sauti za takbira zitokazo kwa majeshi ya Waislamu. Na hiyo ni ahadi isiyo ya uongo, iliyosemwa na Mkweli Msadikiwa (saw) aliposema:




لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ، فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ حَتَّى يَقُولَ الْحَجَرُ: يَا مُسْلِمُ هَذَا يَهُودِيٌّ، فَتَعَالَ فَاقْتُلْهُ

"Mtapigana na Mayahudi na mtawaua kweli kweli, hadi jiwe liseme: Ewe Muislamu huyu hapa Myahudi njoo umuue" (Imepokewa na Muslim)

**Enyi Waislamu:** Hakika wanajeshi katika miji ya Waislamu ni watoto wenu, ni ndugu zenu, ni watu wenu wenyewe, na miongoni mwao wapo wenye ikhlaswi. hivyo basi, waangazieni nyoyo zao kwa haki na muwasukume kwake, ili waikomboe Palestina kutoka kwa umbile la Mayahudi waovu ambao wameinyakua na kueneza humo uharibifu na ufisadi, kwa msaada wa viongozi katika ardhi za Waislamu, ambao badala ya kupigana na huo utawala wa Kiyahudi, wamekua wakichunga usalama wake! Na lau si hivyo, huo utawala haungebakia mpaka leo hii. Kwani hakika Mayahudi hua hawanusuriwi katika vita vya kikweli dhidi ya waislamu.

لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ

"Hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa" [Al-Baqara: 111] Na huu ndio uhalisia wao na hivi ndivyo walivyo. Lakini badala ya kupigana nao viongozi hawa wanafanya nao muamala wa mapatano nao! Na badala ya kuwatoa katika miji yetu kama alivyosema Allah Mshindi Mwenye Hikma:

وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ

"Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni" [Al-Baqara: 191] Mara twaona hawa matwaghut wanathibitsha humo!

قَاتَلَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْفَكُونَ

"Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?"

**Enyi Waislamu:** Hakika mambo yalivyo, hili jambo haliwezi kutengenea ila kwa yale yaliyotengenea mwanzo wake: Nayo ni kuhukumu kwa kwa aliyoyateremsha Allah na wanajeshi watakao watikisa maadui wa Allah. Na hayo hayatokua ila kwa kurudi upya ***Khilafah*** ongofu kwa mwenendo wa Utume, ili ing'oe umbile la Kiyahudi lilochafua Palestina twahara kwa miaka zaidi ya sabini, na hapo kuirudisha Palestina ikiwa kamili katika ardhi za Kiislamu, ikiwa ni mji wa Izza katika serikali yenye Izza, ambayo



ni ***Khilafah*** Iliyo kwa mwenendo wa Utume… na hilo litakuwa tu kwa idhini ya Allah. Na hili latiliwa nguvu na mambo manne yenye maana ya kukatikiwa:

**Kwanza:** Ni kua Ummah wa Kiislamu ni ummah bora zaidi uliotolewa kwa ajili ya watu.

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

"Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu "[Al-i-Imran: 110]. Na ummah ambao hii ndio hali yake,hautavumilia unyonge. Hautoisahau Qudsi yake, haijalishi watakavyofanya matwaghut, bali utawakanyaga kwa miguu yake kisawasawa hasa.

**Pili:** Ahadi itoakayo kwa Allah ya kuwafanya makhalifa katika ardhi.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao*"*[An-Nur: 55] Na bishara ya Mjumbe Wake (saw) aliyobashiri kurudi kwa ***Khilafah*** tena kwa mwenendo wa Utume.

"ثم تكون خلافة على منهاج النبوة"

"Kisha itarudi Khilafah kwa mwenendo wa Utume*"* (Imepokewa na Ahmad)

**Tatu:** Hadithi ya Mkweli Msadikiwa (saw) aliposema kuhusu kupigana na Mayahudi na kuwaua:

" لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ، فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ حَتَّى يَقُولَ الْحَجَرُ: يَا مُسْلِمُ هَذَا يَهُودِيٌّ، فَتَعَالَ فَاقْتُلْهُ"

"Mtapigana na Mayahudi na mtawaua kweli kweli, hadi jiwe liseme: Ewe Muislamu huyu hapa Yahudi njoo umuue) *(Imepokewa na Muslim*)


**Nne:** Chama cha ukweli na chenye ikhlaswi kwa idhni ya Allah, kinachofanya kazi kuhakikisha ahadi ya Allah Mtukufu na bishara ya Mtume wake (saw). Chama ambacho ni kiongozi asiyewadanganya watu wake, chenye uoni na moyo, kinachowaongoza Ummah kwenye kheri ambayo itawafufua kwa Izza na ushindi na kufaulu duniani na akhera na wape habari njema waumini. Hivyo, ummah ambao ndani yake kuna hii mihimili ya ushindi, basi kwa idhini ya Allah

utasimamisha tu *Khilafah* yake na kukomboa Qudsi yake, na utakata mikono ya madhalimu na mabwana wao na wasaidizi wao.

**وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ**

"Na siku hiyo Waumini watafurahi * Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu" *[Ar-Rum: 4-5].*

**27/1/1442H**
**15/9/2020M**
**Hizb-Ut-Tahrir**



instrument inconsistent with this Treaty. For the purposes of this paragraph each Party represents to the other that in its opinion and interpretation there is no inconsistency between their existing treaty obligations and this Treaty. The Parties undertake not to enter into any obligation in conflict with this Treaty. Subject to Article 103 of the Charter of the United Nations, in the event of a conflict between the obligations of the Parties under the present Treaty and any of their other obligations, the obligations under this Treaty shall be binding and implemented. The Parties further undertake to adopt any legislation or other internal legal procedure necessary in order to implement this Treaty, and to repeal any national legislation or official publications inconsistent with this Treaty.

10. **Ratification and Entry into Force:** This Treaty shall be ratified by both Parties as soon as practicable in conformity with their respective national procedures and will enter into force following the exchange of instruments of ratification.

11. **Settlement of Disputes:** Disputes arising out of the application or interpretation of this Treaty shall be resolved by negotiation. Any such dispute which cannot be settled by negotiation may be referred to conciliation or arbitration subject to the agreement of the Parties.

12. **Registration:** This Treaty shall be transmitted to the Secretary-General of the United Nations for registration in accordance with the provisions of Article 102 of the Charter of the United Nations.

Done at Washington, DC, this day Elul 26th, 5780, Muharram 27th, 1442, which corresponds to 15 September 2020, in the Hebrew, Arabic and English languages, all texts being equally authentic. In case of divergence of interpretation, the English text shall prevail.

For the State of Israel:

H.E. Benjamin Netanyahu
Prime Minister

For the United Arab Emirates:

H.H. Abdullah bin Zayed Al Nahyan
Minister of Foreign Affairs and International Cooperation

Witnessed by:

H.E. Donald J. Trump
President of the United States of America

4


ISRAEL-UAE-BAHRAIN NORMALISATION DEAL
UAE and Bahrain agreed to normalise relations with Israel in a historic shift that makes them the first Arab nations to seek official diplomatic ties with Israel since Egypt in 1979 and Jordan in 1994
Palestinian President Mahmoud Abbas slammed the agreement as a "betrayal" of the Palestinian cause - with the Gulf countries reneging on a promise made by Arab states not to embrace ties with Israel until Palestinian statehood is achieved
Jordan signed a peace treaty with Israel in 1994
TURKEY
SYRIA
LEBANON
ISRAEL
IRAQ
IRAN
UAE
BAHRAIN
QATAR
SAUDI ARABIA
OMAN
YEMEN
Egypt signed a peace treaty with Israel in 1979
Israel's Prime Minister Benjamin Netanyahu
Abu Dhabi Crown Prince Mohammed bin Zayed
King of Bahrain Hamad bin Isa Al Khalifa
The US-brokered deal is a huge victory for US President Donald Trump as he seeks a second term on 3 November
For Israeli PM Benjamin Netanyahu, the move is an opportunity to redeem himself amid an ongoing trial for alleged corruption
US President Donald Trump
Source: BBC / Reuters






# Mabadiliko na ushindi wa kweli upo katika kujiunga na ulinganizi wa Khilafah sio makundi ya 'Hustler na Dynasty

Janga la Covid-19 limeleta machungu na afueni kwa Wakenya. Machungu kutokana na makali yanayotokamana janga hilo kuanzia kuangukwa kwa uchumi ambao umepelekea kuzidi kwa ukosefu wa ajira kutoka asilimia 5.2 hadi 10.4 (The Star, 01/09/2020), majonzi kwa jamii kutokana na jamaa kupoteza wapendwa wao, akiba zikimalizika kwa kutafuta matibabu na sehemu za ibada zikifungwa kabisa. Kwa kuongezea, ratiba ya shule ikifutiliwa mbali na kuwaacha washikadau katika elimu wakijumuisha na sio tu wazazi, wanafunzi na walimu wakiwa katika mkanganyiko mkubwa hususan darasa la 8 na kidato cha 4 kwa kuwa vyeti vya KCPE na KCSE huzingatiwa kuwa ni njia ya kufikia fursa nyingi duniani. Ama kuhusu afueni ni kutokana na kusitishwa kwa kelele za kisiasa zilizokuwa zinapanda kila uchao kwa sababu ya wale wanaojiita wapigiaji debe na wapinzani wa BBI. Kwa mara ya kwanza walala hoi na mabwenyenye waliungana katika hofu ya maisha yao licha ya kwamba hali zao ni tofauti kwa kuwa masikini hawezi kumudu gharama ya matibabu na tajiri anaweza kumudu lakini hakukuwa na tiba!

Ama kwa upande wa serikali ya Kenya Covid-19 ilikuwa baraka kwake kwani iliipatiliza ili kushibisha hamu yake ya ulafi na kuzifuata taasisi za kifedha za kiwango cha kieneo na kimataifa ili kuchukuwa mikopo mikubwa kwa kisingizio kuwa inapambana na janga hilo. Kwa upande mwingine, imeisukuma nchi katika kina cha madeni kinachokaribia trilioni Sh.7 hivi karibuni.



Kwa mfano, baina ya Machi na Juni 2020, Kenya ilichukua

jumla ya mkopo wa bilioni Sh.410 takribani bilioni Sh136 kwa mwezi au bilioni Sh.4.5 kwa siku! (Daily Nation, 09/09/2020). Kwa kuwa ule unaoitwa upinzani haupo tena tangu kutokea kwa mkono wa kheri uliofanyika mnamo Ijumaa, 9 Machi 2018. Hivyo basi, serikali ya Kenya inatekeleza sera yoyote inayoitaka pasina wasiwasi kwa kuwa hakuna wakuihesabu.

Njama hadaifu inayoenezwa hivi sasa ni ile ya makundi yanayoitwa hustler, ikiongozwa na William Ruto and dynasty, ikiongozwa na Uhuru Kenyatta, Gideon Moi na Raila Odinga. Raia wanakwenda mbio kujinasibisha na makundi haya. Lakuvunja moyo zaidi ni kwamba makundi haya yanafurahia uungwaji mkono kutoka kwa wale wanaoitwa wanafikra na wasomi! Nukta kiunganishi inayoashiria makundi haya mawili ni kwamba viongozi kutoka kambi zote ni sawa mfano wa mbwa mwitu waliojivika manyoya ya kondoo ili kuweza kuwavizia wengi katika raia ambao hawajazinduka na wanataabika kutokana na maradhi ya UGALI! Maradhi haya ni hatari kwa kuwa yamebuniwa na nidhamu ya elimu ya kisekula ya kirasilimali ambayo msingi wake ni kutotoa fursa kwa watu wenyewe kufikiria kwa kina pasina ushawishi wa kutoka nje kuhusiana na mustakbali wao kwani kimakusudi inawashughulisha kwa kuwa mbioni kutafuta UGALI ili kushibisha njaa yao ya muda mfupi. Hivyo basi, kambi zote mbili sio wageni katika ulingo wa kisiasa bali wamejibadilisha upya ili kuwapatiliza watu kupitia kabila zao. Wao ndio walinzi wa mfumo wa kisekula (wa kutenganisha dini na dola/maisha) wa kirasilimali ambao ndio chanzo cha matatizo mengi yanayoikumba Kenya tangu ‘uhuru bandia wa bendera’ mnamo 1963. Wamejizatiti kutekeleza mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake za sumu zinazojumuisha nidhamu ya kiutawala ya kidemokrasia ambayo inawapa wanadamu uhuru usiokuwa na mipaka na ambayo unasababisha majanga kwa wanadamu, nidhamu ya kiuchumi inayotoa nafasi ya kuchukua mikopo ya kuendelea ya riba na utozaji ushuri unaokandamiza, sera ya kigeni iliyochorwa na mabwana wakoloni ili kulinda maslahi yao, nidhamu ya elimu inayojenga vitambulisho vya kisekula ambavyo lengo lake ni kukidhi mahitaji ya kiviungo n.k. Makundi hayo yanadai




kuwa yanalingania mabadiliko lakini ndani ya sanduku la kisekula la kirasilimali ambalo ndio chanzo cha matatizo sio tu nchini Kenya bali ulimwenguni!

Katika Uislamu, Muhammad ibn Abdullah (saw) alituonya: لاَ يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ "Muumini haumwi mara mbili (na kitu) kutoka katika shimo hilo hilo." (Sahih al-Bukhari 6133). Kama Waislamu tumeshiriki katika "shimo la kidemokrasia" la kubahatisha tangu mnamo 1963 tukitarajia kwamba hali zetu zitabadilika lakini mambo yanazidi kuwa magumu kila kukicha kama vile ukandamizaji na mauaji kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi na misimamo mikali n.k. Mtume (saw) alisema," الْحَلاَلُ بَيِّنٌ وَالْحَرَامُ بَيِّنٌ وَبَيْنَ ذَلِكَ أُمُورٌ مُشْتَبِهَاتٌ لاَ يَدْرِي كَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ أَمِنَ الْحَلاَلِ هِيَ أَمْ مِنَ الْحَرَامِ فَمَنْ تَرَكَهَا اسْتِبْرَاءً لِدِينِهِ وَعِرْضِهِ فَقَدْ سَلِمَ وَمَنْ وَاقَعَ شَيْئًا مِنْهَا يُوشِكُ أَنْ يُوَاقِعَ الْحَرَامَ كَمَا أَنَّهُ مَنْ يَرْعَى حَوْلَ الْحِمَى يُوشِكُ أَنْ يُوَاقِعَهُ أَلاَ وَإِنَّ لِكُلِّ مَلِكٍ حِمًى أَلاَ وَإِنَّ حِمَى اللَّهِ مَحَارِمُهُ "Halali iko wazi na haramu iko wazi, na baina ya hayo yapo mambo yaliyo na shaka (ambayo hayako wazi); wengi katika watu hawajui kama ni halali au haramu. Kwa hiyo yeyote anayewachana nayo ili kulinda dini na heshima yake, basi atakuwa salama na yeyote ambaye atakayeingia katika kitu kutoka kwayo, kisha hivi karibuni atakuwa ameingia katika haramu. Kama vile mtu anavyolisha (wanyama wake) karibu na hifadhi (mpaka), muda si mrefu ataingia ndani yake. Hakika, kwa kila mfalme anahifadhi yake (mpaka), na hakika hifadhi ya Mwenyezi Mungu ni yale Aliyo yaharamisha." (Jami` at-Tirmidhi 1205) na Mwenyezi Mungu (swt) asema: "إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَـٰمُ ۗ Hakika, dini (mfumo) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu" (Aal-Imran 3: 19). Kwa kuongezea, Yeye (swt) asema: وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْكَـٰفِرُونَ "Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri." (Al-Ma'idah 5: 44). Hivyo basi, kujiunga na makundi haya au mengine yaliyobuniwa kwa msingi wa mfumo wa kisekula wa kirasilimali kwa maana vyama vya kiasia ya kidemokrasia imekatazwa kwa mujibu wa Shari'ah ya Kiislamu (Qur'an, Sunnah, Ijma' Sahaba na Qiyas). Kwa kuwa makundi haya yanalingania kumpa mwanadamu nguvu za kupangilia/kutunga sheria ili kusimamia maisha ima kwa kubakisha Katiba ya 2010 iliyoko au kuibadilisha kwa kutumia BBI au njia yoyote ile iliyopo. Hivyo basi, imewafanya watu

kuwa ndio mabwana kwa kuwa itikadi yao ni usekula.

Hakuna shaka kuwa kila mwanaharakati mkweli wa kisiasa anatambua kuwa makundi haya yanapiga njama kwa ajili ya maslahi yao binafsi na yale ya mabwana zao Wamagharibi. Kwa hiyo wanaharakati hao watakuwa wanatafuta mabadiliko ya kweli mbadala ambayo yataweza kuwapa watu ushindi nchini Kenya na duniani kote. Fursa pekee iliyopo ni kujiunga na Hizb ut Tahrir, chama cha Kiislamu cha kisiasa ambacho mfumo wake ni Uislamu. Ni chama cha Kiislamu kilichobuniwa mnamo 1953 na msomi, Sheikh Taqiuddin an-Nabahani (rahimahu Allah) ndani ya Ardhi Tukufu ya Palestina (kuliko na Qiblah cha kwanza cha Waislamu -Msikiti al-Aqsa). Msingi wake ni kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt): وَلۡتَكُن مِّنكُمۡ أُمَّةٌ يَدۡ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ ۚعُونَ إِلَى ٱلۡخَيۡرِ وَيَأۡمُرُونَ ۚ "Na kiwepo miongoni mwenu umma (chama) kinacholingania kwa kheri (Uislamu) na kuamrisha mema na kukataza maovu" (Aal-Imran 3: 104). Hizb ut Tahrir ina lengo moja pekee nalo ni kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Dola ya Kiislamu ya Khilafah ndani ya taifa ambalo limetimiza vigezo muhimu vinavyojumuisha: kwanza-usalama uwe katika mikono ya Waislamu na pili-Shari'ah ya Kiislamu iwe ndio Bwana (inayotumika katika kuwahukumu na kupangilia mambo ya watu). Hizb ut Tahrir haitumii fujo au nguvu kufikia lengo lake.




Mabadiliko na ushindi wa kweli ni kutawaliwa na sheria kutoka kwa Muumba na Mpangiliaji wa ulimwengu, mwanadamu na uhai. Hilo haliwezekani katika hali iliyoko sasa ndani ya dola za kisekula duniani kote. Ni kwa kukumbatia ulinganizi wa kusimamisha Khilafah ndipo wanadamu watakombolewa kutoka katika majanga ya kila siku yanayotekelezwa na makucha ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake mbaya zikisimamiwa na wakoloni Wamagharibi wakiongozwa na Amerika, Uingereza, Ufaransa na washirika wao. Khilafah itawaweka wamwagaji damu wote pale wanapostahili katika debe la taka za historia kwa kuwalipizia kisasi yale waliyowafanyia Waislamu na Uislamu. Wakati ni sasa wa kujiunga na juhudi ambazo zinadhamini amani na utulivu. Kuishi kwetu ni kwa ajili ya kuhakikisha

kuwa jina la Mwenyezi Mungu (swt) liko juu ya kila kitu lakini hivi sasa hali iko kinyume na hivyo ambapo Ukafiri na Makafiri wako juu ya Uislamu na Waislamu. Ilhali Mwenyezi Mungu (swt): وَلَن يَجۡعَلَ ٱللَّهُ لِلۡكَٰفِرِينَ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ سَبِيلاً "wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini" (An-Nisa' 4: 141). Usichelewe, wakati wa kubahatisha umekwisha na sasa ni fursa ya kubadilisha mabaya kwa mazuri kwa kushiriki katika yale ambayo yanayopeana uhai kwa kuitikia anayotuitia Mwenyezi Mungu (swt): يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمۡ لِمَا يُحۡيِيكُمۡۖ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّ ٱللَّهَ يَحُولُ بَيۡنَ ٱلۡمَرۡءِ وَقَلۡبِهِۦ وَأَنَّهُۥٓ إِلَيۡهِ تُحۡشَرُونَ "

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." (Al-Anfal 8: 24). Mfumo wa kisekula na kirasilimali na nidhamu zake zimefeli kupindukia kutokana na ufisadi wake kwa viumbe hai kuliko shamiri ardhini na baharini.

Hii ni fursa ya watu kushindana sio kwa ukusanyaji wa dunia kama tulivyo tahadharishwa na Mwenyezi Mungu (swt): أَلۡهَٰكُمُ ٱلتَّكَاثُرُ *حَتَّىٰ زُرۡتُمُ ٱلۡمَقَابِرَ

"Kumekushughulisheni kutafuta wingi (dunia), mpaka mje (mkishtuka mnapelekwa) makaburini." (At-Takathur 102: 1 - 2). Badala yake tushindane kwa ajili ya kutenda kila kheri hususan kufanya kazi ya kusimamisha Khilafah kwa kuwa ndio mama wa faradhi zote kwa kumuitikia Mwenyezi Mungu (swt): فَٱسۡتَبِقُواْ ٱلۡخَيۡرَٰتِۚ "Basi shindaneni kwa mambo ya kheri." (Al-Mai'dah 5: 48). Huu sio mchakato wa kubahatisha bali ni zoezi adhimu lenye malipo makubwa kwani ni ahadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt): وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّـٰلِحَـٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِى ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ "Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba







atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya wa kabla yao" (An-Nur 24: 55). Kwa kuongezea Mtume (saw) amebashiri kuhusu kurudi kwa Khilafah pale aliposema (saw): ثم تكون ملكاً جبريا، فتكون ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون خلافة على منهاج النبوة، ثم سكت "Kisha kutakuwepo na utawala wa utenzaji nguvu, utakuwepo kwa muda ambao Mwenyezi Mungu atataka uwepo kisha Mwenyezi Mungu atauondoa wakati anapotaka kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume," Kisha akanyamaza. [Ahmad]

Kwa kutamatisha, yale yanayojiita makundi ya 'hustler na dynasty' au mfano wake yanalenga kumkasirisha Mwenyezi Mungu (swt) kwa kudumisha hali iliyoko ambayo inampa mwanadamu nguvu za utungaji sheria kwa kutumia akili yake iliyo na kikomo. Badala yake lazima tufanye kazi turudishe Khilafah ili iwatawale wanadamu kwa msingi wa Shari'ah ya Kiislamu inayotoka kwa Muumba na Mpangiliaji wa ulimwengu, mwanadamu na uhai.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya**

**Habari ya Hizb ut Tahrir**






**ONGEZEKO LA GHARAMA YA MATIBABU NI JANGA LAKUZALIWA NA URASILIMA**

Pindi alipokuwa akieleza uwajibu wa serikali kwa wanainchi wake mjini Kisauni, Dr. Fred Matianagi alisema,***"Wizara inafanya kazi kwa sehemu kama hizi..unaweza kutibitisha kuwa kwa siku nne au tano hujasikia lolote kutoka Kisauni.Jukumu letu sisi ni kusimamia mambo ya watu na hivyo ndio tutakavyo fanya sisi."***

Ni kweli kuwa kazi ya serikali huwa ni kuangalia maslahi ya raia wake na afya ni sehemu ya maslahi haya yalio kalifishwa ndani ya katiba kama miongoni mwa haki msingi.Kwakuwa dola za kirasilima hazitekelezi yale yasemayo, haki msingi ikiwemo hii ya afya imeonekana ni kama mapendeleo hivyo basi kupelekea gharama ya matibabu kuwa tatizo kubwa ulimwenguni.***" Baadhi ya hosipitali za kifahari hapa jijini Nairobi zinatoza ada za juu za kima ksh 200,000 kwa siku na sasa matajiri nao wanapata kuona uzito kujikimu kimatibabu na vile vile kampuni za bima zimejipata kuwa pahali pagumu kwakuwa hazikuwa zimetarajia hali hii ngumu ya kiafya."*** Asema Daktari mmoja kwa mujibu wa hali ya gharama za afya nyakati za janga hili la korona.

Kwa kuangalia afya ni kama mapendeleo,dola zimekuwa zikiekeza fedha na rasilimali kidogo hivyo basi kuruhusu watu binafsi na mashirirka ya bima kuendesha na kubaini sekta ya afya kwa minajili ya kupata faida hivyo basi kuzidisha gharama ya matibabu na afya.

Katika mahojiano na gazeti la Taifa Leo, Daktari Stepehen Ochiel, mwenyekiti wa

kamati ya madaktari alisema kuwa zahanati ni biashara kama vile hoteli. Pindi dola inapo feli kuekeza rasilimali, kichache hufanyika katika kufayanya utafiti na kubuni madawa ndani ya mipaka ya nchi ili kupunguza gharama ya matibabu na hivyo basi kuhifadhi nchi dhidi ya madalali ambao huongeza bei kwa kuangiza madawa na vyombo vya matibabu. Bei hizi zilizo ongezwa baadae hupitishwa kwa mgonjwa hivyo basi kufanya gharama ya matibabu kupanda juu mno. Daktari Ochiel aendelea kusema kuwa mara nyingi watu hukosea  kwa kulinganisha gharama ya matibabu ya humu nchini na ile ya India kwani India huwa yatengeza yenyewe madawa na vifaa ilhali Kenya haitengezi  ila ya agiza kutoka nje kila kitu.

Mkurugezi mkuu wa shirika la afya ulimwenguni Tedros Adhanom Ghebreyesus  baada ya kuona gharama ya matibabu ipo juu hivyo basi kuhisi siku moja huwenda ikaleta tumbo joto kwa nidahamu tawala alikalifisha nchi ziimarishe nidhamu zao zipeane afya kwa watu wote. Maagalizi ya afya kwa watu wote UHC ilibaiiniwa kuwa ndio suluhu kwa tatizo hili la gharama kubwa ya matibabu.

Ama kuhusu UHC, huwa ni yenye kuhitaji  bima , ikimaanisha kuwa afya itaachiwa mashirika ya bima kubaini mwenendo hivyo basi kuzindi kuongeza gharama ya maisha badala ya kupunguza kwani itakuwa kila mwezi zikichukuwa ada ambayo ndio itakayo ruhusu mtu kupata matibabu kwakuwa ndio ada hii hukufanya mwanachama mstahiki bila hivyo huwezi kupata huduma ya afya.

Ama kuangali maslahi ya watu ikiwemo maslahi ya afya ni majukumu ya kiongozi. Asema Mtume SAW,'***'Kila mmoja wenu ni mchungaji na ataulizwa juu ya wale anao wasimamia.Kwa hio mtawala ni mchungaji na ataulizwa juu ya wale anaowatawala.''*** [**Bukhari & Muslim].** Pia alisema Mtume {saw},***''Yule amabae alikuwa mtawala kwa watu kumi ataletwa mbele siku ya kiama huku amefungwa macheni hadi haki na uadilifu imuondoshee mashaka haya au ubepari alokuwa nao umletee maagamivu.''*** **[Tirmidhi]**

Hivyo basi, kwa hali hii tawala ya Khilafah hulazimika kuangalia maslahi ya watu kiasi ya kuwa watu hawakumbwi na shida ikiwemo ukosefu wa matibabu ,gharamu za juu za matibabu na hata kusubiria mda mrefu kupata matibabu.

Nyakati  Umar ibn Abdul Aziz alipokuwa mtawala na kuonekana myonge, kijakazi wake alimuuliza vipi alikuwa myonge na mwenye huzuni. Alijibu Umar,***'' Yeyote alie kuwa kwa nafasi kama hii yangu lazima ahisi hivyo; Lazima ni ajibike na niwape  raia wangu wote***

***haki zao ima kwa wao kuzidai au la."***

Ama kwa hoja ya kuwa Mtume SAW alikabidhi umma daktari ambae alikuwa asli kakabidhiwa yeye,ni wazi kuwa dola ya Khilafah haina budi ila kupeana matibabu ya bure kwa wote.Hali hii inamshurutisha Khalifah kuekeza rasilimali zakutosha kusimamia matibabu ya bure kwa wote.Na iwapo fedha na rasilimali hazitoshi, basi ni fursa kwake kulazimisha kutoza ada kwa matajiri ili kukidhia upungufu wa rasilimali hizo kwa kuwa afya ni shemu ya maslahi ya umma.

Fedha hizo hazita simami tuu matibabu bali pia zita angazia vifaa, majengo, hali ya wafanyikazi wa matibabu, taasisi za kufunza utabibu, mahabara na ilimu ya umma ya matibabu..

Katika zama za Khilafah zahanati na madaktari walikuwa wamewekezwa katika kila miji. Mji wa Baghdad pekee ulikuwa na zahanati sitini zilizokuwa na kitengo cha kutibu wagonjwa wa ndani na wanje pamoja watabibu elfu mmoja. Zahanati za umma kama vile Bimaristan al-Mansu ilikuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa 8,000 huku kila mgonjwa akiwa na wahudumu wawili.Iliwatibu wagonjwa wandani na nje na kuwapa chakula na tiba ya bure.

Nyakati za zama za Khalifah, Al-Muqtadir Billah, kila zahanati ya kugura iliamrishwa itemebelee kila kijiji na ikae kijijini kwa masiku ya kutosha kabla kwenda kijiji chengine.Hii ya dhihirisha kuwa Khilafah itakuwa na zahanati za kugura zitakazo waangalia wale wakaaazi wa vijijini.

Kiongozi wa Khilafah atamchaguwa mkurungezi atakae simamia sekta ya afya na atawaepusha madaktari kufanya kazi ya usimamizi ili wawe na nafasi ya kushughulikia kazi yao ya utabibu. Idara ya afya ita hahikisha imeongeza na kuwa na madaktari waliobobea na wale wakawaida wakutosha kila mahali nchini.Uangalifu pia utakuwa kwa kuhakikisha kunapatikana ubunifu wa madawa kwa kuwashajiisha wanasayansi watafiti kuzidisha kutafuta tiba za maradhi sugu, kujaalia vifaa vyote vya tiba vinapatikana zahanatini, kuwasimamia madaktari katika kazi zao hadi ihakikishwe hamna ufisadi, kuhakikisha thaqafa ya kiisilamu yapatikana kwa wauguzi ili kuhuisha ujajibikaji wao, kuleta mahusiano bora kati ya taasisi za matibabu na vyuo vya matibabu ili mwisho wa kwisha wanafunzi wapate tajiriba bora na mafunzo yao yawe yanaambatana na wakia, kuanzisha sera za kukinga ili kuhifadhi watu dhidi ya maradhi hatari na pia kuanzisha sera bora ya usalama wa kijamii itakayo waangalia wazee, masikini na waathirika.

**Abu Leila**
**Member of Hizb ut Tahrir Kenya**





# VIPI UISILAMU UTAJAALIA VYUMBA ZAIDI KWA WAFU



Kwa kuzidi vifo vinavyotokana na athari za janga la Covd 10, kumekuwa na hofu ya kwamba huenda kukatokea vifo zaidi huku kukiwa na nafasi chache ya kuzikiwa wafu kutokana na kuwa maziara mengi ya umma nchini Kenya yanaenda kujaa. Kwa kusimama na ufahamu huu, familia ya mwenda zake Ursula Buluma ambae alikuwa fanyi kazi wa KPA aliekuwa ni muathirika wa Covid 19 walijihisabu kubahatika pindi walipopata nafasi ya kumzika mwenda zake hapo maziarani mwa Mbarakai kwa ada ya Ksh 6000. ***" Ndio nafahamu maziara ya Mbaraki yanakaribia kujaa lakini kwa sasa hatuko katika janga kwani bado tunayo maziara mengine ambaya yanayo nafasi ziada ya kuzikia."*** Alisema bwana Nato Nyongesa katibu wa Mazingira wa serikali ya jimbo la Mombasa .Ama kuhusu maziara ya makaburini yasemekana ni mwakubwa mjini humo na kwa ajili hio bwana Nyogesa alisema,**"yana nafasi kubwa ila shida yake ni kuwa yamepata changamoto ya kuvamiwa na kujengwa."**

Mnamo tarehe nane Aprili, 2020, Katibu wa Afya Hitan Majevfa wa serikali ya jimbo la Nairobi alikiri kwamba, ***" hamna nafasi katika maziara ya Langata na serikali bado haija pata sehemu badili….tumekuwa tukiwashauri umma ima wazike watu wao bara kwao au katika maziara ya kibinafsi….siku hizi kuchomwa kwa waliokufa kumekubalika na watu nje ya dini ya kihindi….ningeliwashauri watu watumie njia hii ili kuzuia matumizi ziada ya mazishi."***

Isitoshe mnamo mwezi Juni 2, 2015, msimamizi mkuu wa kitengo cha afya Mjini Nakuru,Dr Mungai Kabii aliwahi kutoa notisi kwa maziara ya Nakuru kufungwa.Hii ni baada ya notisi kama



hio kutolewa dhidi ya maziara ya Naivasha na Molo.Ilikuwa

sijambo la siri kuwa maziara ya Nakuru yamejaa na hamna nafasi hali ambayo ili mghadhabisha aliekuwa mbunge wa Bahati wakati huo bwana Kimanai Ngunjiri kulalamika ya kwamba miili sasa imekuwa ikizikwa juu ya mengine na hata mengine ikizikwa njiani ilhali wengine wakiwekeza sementi kwa makaburi ili yasiuzwe.Ingawaje serikali ya jimbo la Nakuru ilidaiwa imetenga ksh million 84 kununua ardhi nyengine, rai ya kuchoma wafu ilikuwa inapigiwa debe kama suluhisho la kudumu la kujaa kwa maziara.Alisema daktari Kabii***,"Wakaazi wameobwa wawe wakichoma maiti zao lakini jambo hili linapata upinzani."***

Tangu mwanaadamu abebe fikra ya kuthamini vitu vya kushikika; masala yanayo husu umauti yamekuwa hayapewi kipao mbele kabisa. Mfumo wa kimaisha wa kuthamini vitu umemfanya mwanadamu kushughulika zaidi na dunia hata kusahau akhera

yake na yale yanayokuja baada ya umauti. Mola asema: * حَتَّىٰ زُرْتُمُ ٱلْمَقَابِرَ أَلْهَىٰكُمُ ٱلتَّكَاثُرُ ***"Munajishughulisha na dunia hadi mauti yanawakuta."TMQ102.1-2.***

Hivo basi hali hii imefanya nchi nyingi za kirasilimali kuwa na matatizo ya kujaa kwa maziara, kunyakuliwa kwa ardhi za maziara na kugeuzwa kwa maziara kuwa nisehemu ya kutupa taka na watu kufanya haja zao ima kubwa au ndogo.

Ama kuhusu sharia zinazo husiana na mazishi, urasilimali umefanya kuwa ni ngumu kupata ardhi badili.Kama ishara ya kughadhabishwa asema daktari Kabii,***"Kupata ardhi kunaonekana kuwa vigumu kwani sharia yaTaifa ya Mazingira yalazimu uchunguzi wa matokeo wa kina mwanzo kabla kukubaliwa na kuidhinishwa na wakaazi wa sehemu ambayo ardhi ya taka kununuliwa kwa minajili ya kufantwa maziara.***" Uzito huu hivyo basi umefanya watu hatiamae kupigiwa debe wa shikamane na uchomaji wa wafu kama suluhu la janga hili.

Kwa kifupi, mfumo wa kirasilimali umeshindwa kupangia maisha ya watu ya kabla na baada ya uhai. Ni mfumo wa kiisilamu pekee ndio unaweza tatua janga hili. Chini ya mfumo wa maisha wa kiisilamu, serikali itakalifishwa kutafuta ardhi zaidi itoshayo kuzika wafu



wote.Kuongezea kwa hilo, fikra ya sadaka endelezi italazimu watu binafsi

wajitolee kuto ardhi zao kwa minajili ya kuzika wafu. Na iwapo kutatokea uhaba wa maziara na hamna ardhi zaidi inapatikana, Uislamu umeruhusu kwa mlango wa dhaarura kuzika watu wawili kwa kaburi mmoja na pia kuzika mtu pahala ambako tayari ashazikwa mwengine kwa sharti kuwa mwili wa aliezikwa awali ushaoza na kupotea na kuwa mchanga, Serikali itahakikisha usalama umeimarishwa maziarani ili kuchunga wenda zao wasikosewe heshima kwa kukojolewa ovyo na nyumba zao kugeuzwa ni sehemu za kutupwa taka na kufanya machafu ya kishirikina na mengineo.Kwa hakika kupitia haya na mengine zaidi ya haya yanayo fungamana na sheria za maiti na maziara,Uisilamu utahakikisha tatizo la kujaa kwa maziara ni janga lililopitwa na wakati na wala kuchomwa maiti sio suluhu lolote lakupendekezwa kwa watu.

**Abu Leila**
**Member of Hizb ut Tahrir Kenya**






**NI SERIKALI YA KHILAFAH PEKEE NDIO ITAKAYO SHIBISHA KIU YA WAFANYI KAZI**

Kufuatia notisi iliotolewa mwezi uliopita ya kufanya mgomo, wauguzi wa nchi ya Kenya ilipofika tarehe 28 Septemba, 2020, walianza rasmi mgomo wao. Wafanyikazi hao 5000 waligoma kutokamana na kucheleweshwa mishahara yao na marupurupu ambayo kwa ujumla ilikuwa ni kiasi cha ksh million 601. Asema katibu wa chama cha wauguzi KNUN bwana Seth Panyaku pindi alipokuwa akiongoza mgomo huo,***"Tunataka taasisi ya SRC iandikie Mkurugezi ikimpa mamlaka ya kutulipa kwasababu twajua pesa zipo.Hatutarudi kazi hadi tupate pesa."***

Tangu kusimama mfumo wakirasilimali, wafanyi kazi wamekuwa hawajapata amani maishani mwao.Kule kwa warasilimali kutaka kuongeza kushibisha mahitaji pasi kutilia maanani maafa ya wafanyi kazi hupelekea kwa mara nyingi kuwepo migomo ya kuitisha malipo mazuri na sehemu bora ya kufanya. Badili yake waajiri nao wamekuwa ni wenye kuwajibu wafanyi kazi kwa kubuni vyama vya wafanyi kazi badili kwa minajili ya kuvunja umoja wao, kuwafuta kazi viongozi wa vyama vya wafanyi kazi,kuajiri majasusi ndani ya wafanyikazi, kukodi wahuni kuwapiga viongozi wa wafanyi kazi na pia kukuza ukabila ili kuvunja ummoja wa wafanyi kazi.

Licha ya kubuni hatua zakutaka kutatua matatizo ya wafanyi kazi kama vile kubuni wizara maalum inayoshughulikia maslahi ya wafanyikazi, kubuni jopo la kushughulikia kukariri mishahara ya wafanyikazi, mfuma wa maisha wa

kiraslimali umekuwa ukifanya hatua hizi ni mzaha zisizo toa suluhu la kudumu.

Historia na hata hisabu za matokeo zaonyesha kwamba hatua kama kubuni mahakama ya kiviwanda, kutambua haki ya kufanya mgomo, ruhusa ya kubuni chama cha wafanyi kazi na zenginezo, zimekuwa ni hatuwa zisizo zaa matunda kwani mwishowe majanga ya wafanyi kazi huo hayatatuki bali wwafanyi kazi ndio wanazidi kufanya kazi mda mrefu bila kupumzika na hata kutopewa marupurupu, wanazidi kucheleweshewa mishahara yao na hata kunyanyaswa kimapenzi, na pia wanazidi kufanya kazi katika mazingira mabaya mno yanayo hatarisha afya zao.

Kwa hakika wafanyik kazi wanahaki ya kupata mishahara mizuri, mazingira mazuri ya kufanya kazi na mahusiano mazuri baina ya muajiri na muajiriwa.Mfumo wa Kirasilimali umefeli kuwapatia matakwa haya wafanyi kazi na ni UIslamu pekee ndio tegemeo lao.




Chini ya Khilafah ambayo ni serikali ya kiisilamu inayotabikisha mfumo wa maisha ya kiisilamu, sheria na sera za ajira za kiisilamu zitatabikishwa vilivyo. Sera za ajira za kiisilamu zitabaini wazi kuwa utukufu na daraja kwa watu ni kwa misingi ya taqwa na wala si mali wala sifa za kiwiliwili. Hili litapelekea kutothamini vitu vya kushikika na pia kuweka pesa ni juu kuliko hadhi ya uwanadamu. Jambo hili huvuja shaksiya ya kimada ambayo huangazia tu manufaa ya kushika potelea mbali mateso wanayo wapata wengine. Isitoshe hii pia itaondoa tabia mbaya dhidi ya wafanyi kazi na hata pia kuwatumia vibaya wafanyi kazi.Kwa hio sera ya ajira ya kiisilamu haita gawa watu kitabaka yaani klasi ya wafanyi kazi na klasi ya wafanyi biashara.Bali itabuni mahusiano mazuri baina ya muajiri na muajiriwa ambayo yatasimama kwa kila mmoja wao kutambua haki zake juu ya mwengine.Isitoshe Uisilamu wabaini ya kwamba makubaliano yasio eleweka yasitabuliwe na yasiwe na mashiko bali kila mmoja atakiwa afahamu makubaliano ili kukinga dhidi ya kutumiana vibaya na kufanyishiana kazi hata nje ya wakati kama vile wafanyi kazi wanyumbani.

Imam Bukhari aeleza kutoka Abu Hurairah (ra), kuwa Mtume saw asema.’’
Allah SWA asema:




**"Kuna watu watata ambao nitawapinga siku ya Hisabu:Mtu ambae anaapa kwa jina langu lakini muongo; Mtu ambae anamuuza mtu asie mtumwa na kisha anakula thamani yake;Na yule ambae anamuajiri mfanyi kazi kisha mfanyikazi akampa huduma yote lakini asimlipe ujira wake."** [Sahih Bukhari, Number 430]

Pia Uisilamu hauta tofautisha baina ya kazi za mkono na za afisi. Hii ni kwasababu zote ni ajira ima kazi inahitaji akili au juhudi ya nguvu kazi.Kama ilivyonukuliwa katika katiba ilioadikwa na Hizb ut Tahrir kwa Khilafah tarajiwa, kifungu cha 154 chaeleza.**''Wafanyi kazi wa kampuni na wale wa kujiajiri wana haki sawa kama wale walioandikwa na serikali.Kila yule anaefanya kazi kwa badili ya ujira, pasi kutilia maanani kazi anayo fanya anatambulika kuwa ni mfanyikazi…''** Kwa hakika sera kama hii itahakikisha mfanyikazi yeyote anahaki ya likizo kama mfanyi kazi mwengine.

Kwa kweli hatua nyingi zitawekwa na serikali za kirasilimali ili kukabili majanga ya wafanyi kazi lakini kwa kuwa hatua hizi msingi wake ni akida fisidifu, majanga ya wafanyi kazi yataendelea kuwapo bila tatuzi.Wafanyi kazi lazima watambue uovu wa urasilimali, na pindi watakapo tambua hilo basi rai ya nguvu ya uuma itaamka na kuita mwito wa mabadiliko ambao mwito huo hautazuilika.Kwa kweli nguvu ya wafanyi kazi ni ya ajabu.

**Abu Leila**
**Member of Hizb ut Tahrir Kenya**

# Jarida la UQAB



uqab.or.ke uqab_htk UQAB-Magazine-1911964012162253